# UFUTUHI WA KIAFRIKA: NADHARIA MPYA YA KUSHUGHULIKIA TAALUMA ZA KI-INSIA

*Athumani S. Ponera*

**Ikisiri**

*Makala hii inawasilisha jaribio la kuifafanua nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika kama nadharia mpya yenye uwezo wa kutumika kushughulikia masuala ya ki-insia. Taaluma za ki-insia, katika makala hii, zinamaanisha shughuli kama vile tafiti na tahakiki zinazofanywa kwenye nyuga zinazohusiana na lugha, sanaa, historia, falsafa, na utamaduni. Kwa kipindi kirefu, taaluma kama hizi zinazowahusu Waafrika zimekuwa zikishughulikiwa kwa kutumia viunzi vya nadharia vyenye asili na mwegamo wa maeneo ya nje ya jamii za Kiafrika. Hali hii, kwa namna moja au nyingine, husababisha upungufu katika kupata majibu ya matatizo yanayoshughulikiwa. Katika kuitikia wito kwa wanataaluma wa Kiafrika kutafuta na kutumia nadharia zenye asili na mwegamo wa jamii husika, makala hii inaitambulisha dhana ya Ufutuhi wa Kiafrika kama nadharia yenye uwezo wa kuwa Kiunzi cha Nadharia[8] chenye uwezo wa kuendeshea taaluma za ki-insia.*

## Utangulizi

Kuna orodha ndefu za nadharia ambazo zimekuwa zikitumiwa na watafiti na wachambuzi wa masuala mbalimbali yanayohusiana na lugha, fasihi na nyuga nyingine za ki-insia kama viunzi vya kuendeshea shughuli zao. Hata hivyo, sehemu kubwa ya nadharia hizo haina asili wala ukaribu mkubwa na jamii zilizozizaa au zinazoelekezewa mambo au kazi husika zinazoshughulikiwa. Kuna umuhimu mkubwa wa kutumia nadharia ambayo ama asili yake inaendana (iendane, siyo lazima sana ifanane) na mazingira ya jambo au kitu kinachoshughulikiwa; au kiwe na namna fulani ya ukaribu na mazingira hayo. Umuhimu huo unachagizwa na hoja mbalimbali. Miongoni mwazo ni kuwapo kwa tofauti kati ya fasihi ya jamii moja na nyingine. Mlama, katika Mutembei (2012:vi), anaitilia nguvu hoja hii kwa kusema: “Fasihi ya Afrika ni tofauti na fasihi ya jamii nyingine...”. Tofauti

[8] Dhana ya ‘Kiunzi cha Nadharia’ inadokezwa hapa kwa kutofautishwa na dhana ya ‘nadharia’. Kiunzi cha nadharia hurejelea uhusiano baina ya nadharia na mazingira ya utumiwaji wake. Kwa maneno mengine, humaanisha ruwaza maalumu ya utumiwaji wa nadharia katika kuendeshea jambo fulani (Ponera, 2016; Tavallaei na Abu-Talib, 2010).

zinazozungumziwa hapa zinahusu vipengele vya kiujumi, kihistoria, kiutamaduni, kidhamira, na kijamii.

**Dhana ya Nadharia**

Ponera (2016:129) anamnukuu Tavallaei na Abu-Talib (2010:572) ambaye anaielezea dhana ya nadharia kwa namna tatu ambazo ni:

> Mosi, nadharia huweza kumaanisha seti ya kanuni na maelezo kuhusu jambo fulani. Pili, huweza kuchukuliwa kama lensi au dira ya kuendeshea tafiti, tahakiki, na/au mijadala. Tatu, ni nyenzo ya kufikia mahitimisho ya kimjadala kuhusu dhana mbalimbali za sayansi za jamii.

Namna hizi za kuielezea nadharia hutegemea vigezo vya eneo/uga wa kitaaluma pamoja na zama za nyakati mbalimbali. Takribani nyuga zote zinazozungukia maisha ya mwanadamu zina nadharia zake. Wafula na Njogu (2007) wanabainisha kuwa nadharia, kwa kigezo cha kimuundo, huweza kuwekwa katika makundi matatu. Nayo ni: nadharia asilia (ambayo haina uhusiano na nadharia nyingine yoyote); nadharia nyambuzi (ambayo imepanuliwa kutokana na nadharia nyingine); na, nadharia changamano (ambayo huundwa na nadharia mbili au zaidi).

Wafula na Njogu (whj.) wanaendelea kutongoa sifa za nadharia nzuri. Wanadai kuwa nadharia nzuri ni ile ambayo: (i) imefanyiwa majaribio na uchunguzi mwingi; (ii) ina sifa ya kimfumo; (iii) iwe na maelezo ya kiutondoti; (iv) iwe na manufaa kwa yeyote anayetaka kuitumia; na, (v) iwe ina uwezo wa kukubali minyumbuko na/au mabadiliko pale inapobidi (uk. 11). Tavallaei na Abu-Talib (2010) wanaongezea kuwa nadharia nzuri ni ile yenye kufafanua kiutondoti vipengele muhimu vitatu ambavyo ni **dhana**, **misingi** au **mihimili**, na **uelekeo**. Kwa msingi wa kinadharia, dhana ni kipashio kidogo zaidi kinachoelezea fikra inayojipambanua kwa namna mahsusi. Nadharia moja huweza kuwa na fikra (dhana) nyingi lakini zinazoelekeana. Msingi au mhimili ni muunganiko wa dhana mbalimbali. Dhima kuu ya msingi au mhimili wa nadharia fulani ni kuishikilia nadharia husika. Nadharia moja huweza kuwa na misingi au mihimili kadhaa. Uelekeo hupatikana kutokana na mkusanyiko wa dira (maana za jumla) zinazobebwa na misingi au mihimili ya nadharia. Hii inamaanisha kuwa, kutokana na dira za mihimili ya nadharia husika, mtumiaji hupata uelekeo wa jinsi ya kulitazama na kulifafanua jambo au tukio fulani. Kwa hiyo basi, dhima kuu ya nadharia, chambilecho Johnson na Christensen (2008), ni kuchanganua 'vipi' na 'kwa nini' mambo hutokea kwa jinsi yatokeavyo katika miktadha husika.

Kuhusu kuzuka kwa nadharia, Khamis katika Mutembei (2012) na Wamitila (2003) wanadai kuwa nadharia huzuka kufuatana na miktadha inayohusiana na jamii.

Khamis (khj) anasisitiza kuwa nadharia huzuka pasi na ukomo... Na kwamba, hakuna nadharia iliyodumu milele, kwani hatimaye nadharia yoyote huweza kufikia mazingira ya kukwama katika kuchanganua kazi husika kisayansi (uk. vii). Fikra hizi zinatuleta katika uhalisi wa matumizi ya nadharia zenye asili ya nje ya Afrika kama viunzi vya kuendeshea masuala yanayowahusu Waafrika.

**Dhana ya Ufutuhi kwa Ujumla**

Ufutuhi ni dhana unde iliyoibuliwa na Ponera (2010) kutoka katika dhana mama ya 'futuhi'. Imeshadidiwa na Juma (2014), na Ponera (2014a, 2014b, na 2016). Ponera (2010) ameiunda dhana hii ya ufutuhi na kuipa upanuzi huo, kisha kupendekeza itumiwe kwa mawanda ya namna mbili, mawanda finyu na mawanda mapana. Anaelezea kuwa, kwa mawanda finyu, ufutuhi hujielekeza katika hali ya matokeo matatu yanayotokana na vipengele mbalimbali vinavyohusiana na unyemi. Vipengele hivyo ambavyo anaviita vijenzi ni kama vile kejeli, ufyosi, dhihaka, vijembe, na utani. Matokeo matatu yanayorejelewa hapa ni kicheko, ucheshi na furaha. Kwa mawanda mapana, hujumuisha kwa pamoja vijenzi, miktadha ya utokeaji, pamoja na matokeo.

Inafahamika kuwa dhana hizi ambazo makala hii inazitambulisha kama vijenzi ndizo zilizozoeleka sana katika maandishi ya kitahakiki na kitafiti katika taaluma za fasihi. Mbali na dhana hizo tatu za kicheko, ucheshi na furaha, dhana nyingine inayoelekeana na ufutuhi ni jelotolojia. Tungeweza kupendekeza matumizi ya dhana hii badala ya kutumia ufutuhi, hata hivyo, etimolojia ya jelotolojia, kama wasemavyo Fry na Allen (1998), imejengwa na maneno mawili ya lugha ya Kiyunani; nayo ni *gelos* lenye maana ya kicheko, na *ology* linalomaanisha taaluma. Kwa hiyo basi, jelotolojia ni taaluma inayochanganua maana, aina, utokeaji, historia, mawanda, upokezi pamoja na athari za kicheko. Hata hivyo, kumekuwa na mkanganyiko mkubwa wa kimatumizi kwenye dhana hii ya jelotolojia; ambapo, wakati mwingine hutumiwa kumaanisha michakato yote ya ki-futuhi.

Kwa hiyo, hoja muhimu zilizotumiwa na Ponera (khj) kuitumia dhana ya ufutuhi badala ya dhana nyingi zilizozoeleka ni:

a) Kuwapo kwa mwingiliano wa kimaana katika vijenzi na matokeo ya vipengele mbalimbali vinavyohusiana na kicheko, furaha, na ucheshi taz. Ponera (2014a); na

b) Kutii kaida ya asili ya namna ya kuzitumia au kuzichukulia dhana zote zinazohusiana na kicheko, furaha, na ucheshi. Hapa inamaanisha kuwa mdhihiriko wa vijenzi na hatua zinazotuelekeza kwenye vipengele vitatu maarufu vilivyotajwa katika hoja (a) hapo juu hutokea na hutumiwa kwa

namna ya jumla, siyo ya kiutengano. Hoja hii inatiliwa nguvu na Chimerah anayenukuliwa na Ponera (2014a:19) akisema:

> ...hivyo vyote (vijenzi vya ufutuhi) huwa havibaguliwi katika matumizi ya lugha. Katika fasihi, huwa tunavitenga na kuvibagua. Kwa mfano, tutazamapo filamu au tamthiliya ikiigizwa jukwaani, ni vigumu sana kusema 'sasa hapo ni kejeli' au 'hilo sasa ni fumbo' ~~n.k~~. Hizi ni mbinu zinazopatikana katika lugha kulingana na tamaduni zao. Zote huwapeleka watu katika kucheka au kufurahi. Wanafasihi tumezipa majina hayo ili tuweze kuzielewa kwa urahisi zaidi. Hivyo, wazo la kuvijumuisha vipengele hivyo kimatumizi kupitia hiyo istilahi ya ufutuhi ni sahihi; hiyo ni sawasawa na kurudi katika asili ya matumizi sahihi ya lugha[9].

Ukweli wa fikra hizi unaweza kuthibitishwa tunapomakinikia maana, hatua, mipaka, miktadha ya utokeaji au utendekaji, na matokeo ya vipengele kama vile utani, dhihaka, stihizai, kijembe, tashtiti, na ufyosi. Kilicho bayana ni kwamba, pamoja na tofauti ndogondogo za kimaana na kimipaka, kuna mwingiliano mkubwa wa miktadha ya utokeaji au utendekaji pamoja na matokeo ya vipengele hivyo (taz. Ponera, 2014a). Hoja hizo zote zinatuyakinishia haja ya kuitumia dhana jumuishi ya ufutuhi ili kutoa maana za mawanda yote mawili kama ilivyokwishabainishwa hapo juu.

Utokeaji na/au utendekaji wa masuala ya kifutuhi hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, na kutoka jamii moja hadi nyingine. Hii hutokana na sababu zifuatazo:

a) Tofauti ya hifadhi ya maarifa (kumbukumbu) juu ya jambo au kitu fulani: utokeaji wa ufutuhi hutegemea sana na kiwango cha kukumbuka jambo lililokwishasajiliwa ubongoni na kuhusisha jambo hilo na jambo jipya linalowasilishwa;
b) Tofauti ya hali na mwelekeo wa kisaikolojia wa mtu au watu wanaowasilishiwa ufutuhi;
c) Tofauti ya utamaduni: mathalani, jambo ambalo linaruhusiwa kutumiwa na jamii fulani katika kufanyia futuhi laweza kuwa sehemu ya miiko katika jamii nyingine;
d) Tofauti za kiidili[10]. Kila jamii ina idili zake maalumu zinazotawala namna yao ya kuishi;

---

[9] Mahojiano baina ya Rocha Chimerah na mwandishi wa makala yalifanyika Agosti 28, 2013 jijini Nairobi. Chimerah ni Mhadhiri Mwandamizi wa taaluma za Fasihi.

[10] Idili ni jumla ya nguzo-msingi au vigezo ambavyo jamii hujiegemeza kwavyo kama vipimo vya kuhakikia au kulinganishia uzuri au ubaya wa jambo. Kila jamii na kila kipindi

e) Tofauti za miktadha ya utokeaji na/au utendekaji;
f) Tofauti za mahusiano ya kijamii baina ya mtu mmoja na mwingine au tofauti za kikaida kati ya jamii moja na nyingine; na
g) Tofauti za malengo au matumizi ya ufutuhi wenyewe.

Hoja hizo za kuwapo kwa tofauti za ufutuhi zinatufunulia ukweli kuhusu kuwapo kwa ufutuhi wa jamii mbalimbali. Kwa mfano, kuna ufutuhi wa Kiyunani, ufutuhi wa Kiamerika, ufutuhi wa Kijapani, Ufutuhi wa Kiasia, na ufutuhi wa Kiafrika. Hii inaonesha kuwa kuna sifa pambanuzi zinazoujenga ufutuhi wa kila eneo, na hivyo, kujitofautisha na ule wa eneo jingine.

**Ufutuhi wa Kiafrika: Kama Dhana na Nadharia**

Ufutuhi wa Kiafrika, kwa jicho la kidhana, ni jumla ya mazingira na vipengele vyote vinavyohusika na kutokea kwa kicheko, furaha na ucheshi unaoendana na Waafrika. Makala hii inaitaja dhana ya Waafrika huku ikitambua kuwapo kwa upana wa kimaana wa dhana yenyewe. Hii ni kutokana na kuwapo kwa uwingi na mwingiliano wa sifa za kuwapambanua. Kwa mwelekeo wa makala hii, dhana ya Waafrika inarejelea jamii zote za watu wenye rangi nyeusi wanaopatikana katika maeneo yote ya Afrika nje ya ukanda wa Kaskazini (Ukanda wa Waarabu) na Pembe ya Afrika. Hivyo, tunazirejelea jamii za Magharibi mwa Afrika, Mashariki mwa Afrika, Katikati mwa Afrika, na za Kusini mwa Afrika. Ni imani yetu kuwa maeneo haya yana namna fulani ya kuendana kwa mienendo ya jumla ya tamaduni, falsafa na ujumi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa dhana ya ufutuhi ina ukaribu mkubwa na vipengele hivyo vitatu—utamaduni, falsafa na ujumi.

Hivyo, ufutuhi wa Kiafrika ni ule unaotendwa na kudhihirishwa na Waafrika wenyewe, ukisawiri vipengele vya maisha yao, na kuelekezwa kwenye shabaha zinazofungamanishwa na falsafa yao. Hapa, hoja ya msingi ya makala hii ni kwamba, katika umbo na namna yoyote ambayo ufutuhi wa Kiafrika utaegemezwa na kudhihirishwa (kama vile maandishi, michoro, matendo, na uneni [wa ngazi ya tungo au matini ndefu]), ni lazima utakuwa unatumia lugha, mazingira, hali na vipengele vingine vinavyohusiana moja kwa moja na Waafrika wenyewe.

Mpaka hapa, swali linaloweza kuibuliwa ni kuwa: je, **ufutuhi una sifa ya kuwa nadharia inayoweza kutumika kama kiunzi cha kushughulikia masuala ya ki-insia?** Jibu la swali hili muhimu linaelekezwa katika kumulika sifa za nadharia. Imekwishadokezwa hapo juu na Njogu na Wafula (2007) na Tavallaei na Abu-Talib (2010) kwamba, nadharia huonwa kama umbo timilifu linalobeba sifa

kina idili zake ambazo hutumika kupimia thamani ya vitu au masuala mbalimbali (Ponera, 2014c:22).

zilizobainishwa. Miongoni mwazo ni kuwa imefanyiwa majaribio na uchunguzi mwingi, kuwa na sifa ya kimfumo, kuwa na maelezo ya kiutondoti, kuwa na manufaa kwa yeyote anayetaka kuitumia, na kuwa na uwezo wa kukubali minyumbuko na/au mabadiliko pale inapobidi. Sifa nyingine ni kufafanua vyema vipengele muhimu vya ‘dhana’, ‘misingi au mihimili’ pamoja na ‘uelekeo’. Kwa ujumla, sifa hizi zimegawanyika katika makundi makubwa mawili. Nayo ni sifa zinazopaswa kuonekana toka awali; na zile endelevu zinazopaswa kuonekana wakati nadharia tayari imekwishakutambulishwa. Kuhusu sifa zinazopaswa kuonekana toka awali, ufutuhi wa Kiafrika unaonekana kuwa nazo kwa kiasi cha kutosha. Hizi ni kama vile umfumo, utondoti wa kimaelezo, manufaa, pamoja na kuwa na dhana, misingi na uelekeo.

Nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika ni umbo la kinadharia linalojitosheleza kwa kuwa na vipengele vyote hivyo. Kuhusu dhana, ufutuhi unaundwa na dhana kama vile kejeli, stihizai, vijembe, utani, tashtiti, na ubeuzi (hizi zipo chini ya anwani ya vijenzi vya ufutuhi). Pia, kuna dhana za ucheshi, furaha (unyemi) na kicheko (hizi zipo chini ya anwani ya matokeo ya ufutuhi). Zaidi, zipo dhana za unyume, balagha, utanakuzi, majazi na utwezaji (hizi zaweza kufafanuliwa chini ya anwani ya aina au makundi ya ufutuhi). Dhana nyingine ni msigano, ujikwezaji (mkwezo) na burudiko (hizi huweza kufafanuliwa chini ya anwani ya mikabala inayoelezea chanzo au ujitokezaji wa ufutuhi). Hivyo, kwa upande wa kuwapo kwa dhana, inadhihirika kuwa dhana ya ufutuhi kama umbo la kinadharia inajitosheleza kwa kuwa na dhana zinazoweza kujenga misingi au mihimili.

Kwa upande wa misingi au mihimili, ufutuhi wa Kiafrika una sifa zake maalumu ambazo zinaupambanua. Kwa upande mwingine, sifa hizo zinaweza kusimama kama misingi au mihimili ya kuutazama ufutuhi huo. Sifa hizo ni:

a) Hutumia lugha nyepesi au matendo yenye viashiria vya wazi;
b) Hutumia vijenzi vya tashtiti kama vile vitanza-ndimi, vina, na uradidi wa mambo (takriri) ili kuleta mnato na/au mvuto;
c) Humlenga mwanadamu moja kwa moja. Hata pale sura ya nje inapohusisha viumbe wengine nje ya mwanadamu, kwa ndani humhusu mwanadamu. Mihalcea na Pulman (ht) wanaifafanua zaidi dhana hii kwa jicho la kiisimu; wanadai kuwa tungo au matini zenye ufutuhi mara nyingi hutawaliwa na vipashio vya nafsi vinavyomwelekea moja kwa moja mtu fulani;
d) Hutumia vionjo vya ubwege kama vile mazungumzo ya kubwabwaja na vitendo visivyoeleweka-eleweka (visivyo na mantiki iliyo bayana), pamoja

na mwonekano wa hovyo-hovyo kwa wahusika katika vipengele vya mavazi na maumbile kwa jumla;

e) Hutawaliwa na unyume (kupitia kupindua uhalisi wa jambo); na
f) Hutumia namna mbalimbali za ufyosi (matusi) na vionjo vingine vya maneno yanayoelekezwa zaidi katika maneno yanayohusu katikati ya mwili wa mwanadamu (viungo na matendo ya siri kama vile ngono, na kujisaidia). Eneo linalofuatia kuelekezewa vionjo hivyo ni usoni.

Sifa hizi zinatudokezea kuhusu kuwapo kwa kona muhimu zinazoishikilia dhana ya ufutuhi. Hii inamaanisha kuwa, ikiwa mtu analenga kulitazama jambo au kitu chochote kwa jicho la kiufutuhi, anaweza kutumia sifa hizi kama nyenzo za kumwongoza au kusimamia.

Dira au uelekeo wa nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika hubainika wazi kupitia sifa au mihimili iliyodokezwa hapo juu. Sifa hizo zikimakinikiwa kwa pamoja au sehemu yazo zinatupatia maoni yafuatayo ya ki-dira au ki-uelekeo kuhusu namna ya kulichukulia au kulitazama jambo kwa kutumia nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika:

a) Kila jambo au kitu kina maana na mitazamo miwili au zaidi. Hivyo, ni vema jambo likachunguzwa kwa kina sura zake za nje na ndani kabla ya kuliwekea hitimisho;
b) Binadamu, hasa awapo katika muktadha wa kundi na wenzake, wakati wote yumo katika harakati za kutafuta ‘vilainishi’ vya ugumu wowote anaokumbana nao katika maisha. Hali hii huifanya dhana ya ufutuhi kuwa ‘zana’ muhimu ya kuendeshea maisha;
c) ‘Hakuna tupu iliyo tupu’. Hii inamaanisha kuwa jambo lolote katika ulimwengu huu lina maana yake; yaani, hata pale panapodhaniwa hapana kitu chochote pasidharauliwe. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, mahali hapo lazima pana angalau ‘hewa’ ambayo ni sehemu mojawapo ya maada (*matter*). Kwa muktadha wa nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika, vipengele vinavyoweza kuonekana kama vile vya kupitwa tu katika matini ya kifasihi, kama vile ubwege (utendaji na unenaji wa mambo kwa namna ya kubwabwaja au hovyo hovyo), huwa vinabeba tunu nzito iliyofichwa ndani yake. Ni kazi ya wahakiki au/na watafiti kuifichua; na
d) Hakuna namna moja ya kulipokea jambo, hususani upokezi wa ladha ya ujumi wake. Kila mmoja ana misingi yake ya kupokea na kufaidi kilichomo ndani ya jambo husika.

Kimfumo, nadharia hii imejikamilisha kutokana na kuwapo kwa dhana na vipengele mbalimbali vinavyotofautiana hadhi, ngazi na dhima, bali vinahusiana na

kushirikiana katika kuijenga nadharia yenyewe. Mfano mzuri hapa ni vipengele vya dhana, misingi na dira ambavyo vimefafanuliwa hapo juu.

Sifa endelevu ambazo zinapaswa kuonekana wakati nadharia tayari imekwishakutambulishwa ni pamoja na kufanyiwa majaribio na uchunguzi mwingi pamoja na kuwa na uwezo wa kukubali minyumbuko na/au mabadiliko pale inapobidi. Hizi zinahitaji muda; yumkini, nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika itajalizwa na sifa hizi kadri muda utakavyosonga mbele huku ikitumiwa.

**Matumizi ya Nadharia ya Ufutuhi na Taaluma za Ki-insia**

Dhana ya *insi* etimolojia yake ni katika lugha ya Kiarabu. Kwa Kiswahili, neno hili linazungukia maana za 'mtu', 'mwanadamu, na 'utu'. Kwa jumla, humaanisha 'mtu', '-a mtu', au '-a kiutu'. Hivyo, taaluma za ki-insia, kama ilivyodokezwa mwanzoni mwa makala hii, ni zile zenye mfungamano wa karibu sana na mwanadamu au shughuli zinazoyajenga maisha yake. Taaluma hizo ni zile zinazohusiana na nyuga kama vile lugha, sanaa, historia, falsafa au utamaduni. Nyuga hizi zina masuala au vipengele vingi ambavyo hushughulikiwa na wataalamu katika shughuli za uhakiki, mijadala, pamoja na tafiti. Baadhi ya masuala au vipengele hivyo ni mivigha (kama vile jando na unyago), sanaa za maonesho (kama vile matambiko, michezo ya watoto na majigambo). Vipengele vingine ni mahusiano ya watu katika jamii (kama vile vijenzi, matokeo, na nadharia mbalimbali za ufutuhi), matumizi ya lugha pamoja na tabia na mienendo ya wanajamii. Zaidi ya hivyo, kuna vipengele vya tarihi na historia za mtu au jamii pamoja na makundi mbalimbali ya falsafa ambavyo pia vinaweza kushughulikiwa kwa kutumia nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika.

Miongoni mwa sifa za jumla za vipengele hivi vilivyotajwa kuwa ni vya ki-insia ni: Mosi, kujiambatisha kwa karibu na maisha ya mwanadamu; hivyo, kuchangamana zaidi na vipengele vya utamaduni na kaida nyingine za maisha. Pili, kuwa na tofauti na/au unyumbufu wa kiasi kikubwa cha jinsi kipengele husika kinavyojidhihirisha au kutendeka katika jamii moja na nyingine. Tatu, kubebwa na upekee na/au usiri wa namna fulani katika kaida zake za uendeshaji. Sifa hizi zinatuyakinishia hoja na haja ya kuhitajika kwa nadharia yenye ufungamano wa karibu na mwenendo wa maisha ya kila siku ya wanajamii ili kuweza kushughulikia masuala kama haya. Hii, hatimaye, itawasaidia wahakiki, watafiti na wasomaji wa kawaida kuwa katika mazingira mazuri na mepesi ya kufikia majawabu na mahitimisho murua. Miongoni mwa nadharia hizo ni Ufutuhi wa Kiafrika; ambapo, mhusika (mtafiti, mhakiki au hata msomaji wa kawaida) anaweza kuteua baadhi ya misingi ya nadharia hii ili kumsaidia kuchimbua jambo analolishughulikia na kulipatia maana.

## Hitimisho

Makala hii imefanya jaribio la kuitambulisha nadharia mpya ya Ufutuhi wa Kiafrika. Hoja ya msingi ya makala ni kwamba, hii ni mojawapo ya nadharia chache zinazoweza kuyashika na kuyashughulikia hadi kwenye uketo masuala yanayotokana na/au kuwahusu Waafrika. Hii yatokana na ukweli kuwa nadharia ya Ufutuhi wa Kiafrika inatokana na kaida na falsafa za Waafrika wenyewe. Kwa hiyo, makala inatoa wito kwa watafiti, wahakiki na wasomaji wa kawaida (wa jamii na kazi zinazohusiana na Waafrika) kuanza kuitumia nadharia hii katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na masuala ya ki-insia ili kurahisisha upatikanaji wa majibu.

## Marejeleo

Fry, W.F., & Allen, M. (1998). *Creating Humor: Life Studies of Comedy Writers* (2nd Edition.). New Brunswick: Transaction Books.

Johnson, B., and Christensen, L. (2008), *Educational Research: Quantitative, Qualitative, and Mixed Approaches*, SAGE Publications, Thousand Oaks, CA.

Juma, S. (2014). "Ufutuhi katika Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo", Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Mihalcea, R. na Pulman, S. (ht). 'Characterizing Humour: An Exploration of Features in Humorous Texts'. Iliyosomwa katika https://www.cs.ox.ac.uk/files/244/mihalcea.cicling07.pdf tarehe 15/02/2018.

Mutembei, A.K. (2012). *Korasi katika Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Ponera, A. S. (2010), "Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa, na Athari Zake kwa Wasomaji," Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2014a), "Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi", Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2014b). 'Kutoka Futuhi hadi Ufutuhi: Chimbuko, Maendeleo na Nadharia Zake', katika *Mulika* na. 33, Mulokozi, M.M. na Hans, M.M. (Wah.), kur. 1-20.

Ponera, A. S. (2014c). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Ponera, A.S. (2016). 'Suala la Matumizi ya Nadharia kama Kiunzi cha Tatifi za Kitaamuli: Mfano wa Matumizi ya Nadharia ya Ukanivali' katika *Journal of humanities (JH)*, Chuo Kikuu cha Dodoma, Volume 3(1), kur. 128-143.

Tavallaei, M. na Abu-Talib, M. (2010), "A General Perspective on Role of Theory in Qualitative Research", *The Journal of International Social Research*, Vol. 3, No. 11, 570-577.

Wafula, R. Na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.